

Jina.....  
Shule.....

Nambari yako.....  
Sahihi yako.....  
Tarehe.....

102/3  
KISWAHILI  
FASIH  
KARATASI YA 3  
Saa 2  $\frac{1}{2}$

**TEN NOTCH EXAM MERIT TWO (PRE-MOCK) 2016  
KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION.**

**MAAGIZO**

- (a) Jibu maswali manne pekee
- (b) Swali la kwanza ni la lazima.
- (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:  
Tamthilia, Hadithi Fupi, Fasihi simulizi na Riwaya
- (d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- (e) Andika kila jibu kwenye ukurasa mpya.

*Karatasi hili ina kurasa 4 zilizopigwa chapa  
Watahiniwa wanastahili kuhakikisha kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

**A: USHAIRI**

**1. Lazima**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,  
Merejeya kwa miradi, kuhitimisha dhamira,  
Kukejeli va budi, niwafunze utu bora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Sirikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,  
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,  
Yamini kuwa gaidi, wakitupora mishahara,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana kifikra,  
Wana yao maksuudi, kujizombea ujira,  
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,  
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,  
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Maskini watozwa kodi, wapwani na walo bara,  
Kwa uvumba na uudi, mwawalipa kwa hasara,  
Hamudhamini miradi, mejihisi masogora,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,  
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura,  
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,

Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,  
Kuwachuja al muradi, kwa za mkizi hasira,  
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

**Maswali**

1. (a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili (alm1)  
(b) Ainisha shairi hili kwa jinsi tatu na kutoa sababu. (alm3)  
(c) Onyesha mbinu za lugha katika shairi hili. (alm2)  
(d) Ainisha matumizi matatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (alm3)  
(e) Ika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi. (alm4)  
(f) Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alm3)  
(g) Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. (alm1)  
(h) Eleza muundo wa shairi hili. (alm3)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

Said A. Mohamed: *Kidagaa Kimemwozea*

Jibu swali la 2 au la 3

2. 'Alaa ! Mtoto mdogo hata ubwabwa haujakutoka shingoni unakimbilia nini..... ?' (alama 4)
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 2)
  - b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondoo.
  - c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha kwamba kwa hakika ubwabwa ulikuwa umemtoka shingoni anayerejelewa (alama 6)
  - d) Asasi inayorejelewa katika muktadha huu inakumbwa na matatizo mengi. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili matatizo yoyote manne kwa mifano mwafaka (alama 8)
3. Kifo cha Uhuru ni jazanda ya hali ya mambo katika jumuiya ya kidagaa kimemwozea. Thibitisha. (alama 20)

**C: HADITHI FUPI**

4. Diwani ya Damu Nyeusi imesheheni jamii ya watu dhulumati. Jadili ukirejelea hadithi za:
  - (a) Maskini, Babu Yangu. (alama 20)
  - (b) Mwana wa Darubini.

**NDOA YA SAMANI**

5. "Chamblecho Waswahili atafutaye hachoki, na akichoka keshapata." (alama 4)
  - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 16)
  - (b) Fafanua mtazamo wake Abu kuhusu maisha.

**SEHEMU D: TAMTHILIA**

**MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)**

**Jibu swali la 6 au7**

6. "Tunaweza kutangaza katika vyombo vya habari. .... Watu wengi huko nje wana njaa."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

(alama 4)

(b)

(c) Fafanua sifa mbili za mzungumzaji wa dondoo hili.

(alama 2)

(d)

(e) "Hali inayoipata Cheneo katika muktadha ambambo dondoo hili limekitwa ni msiba wa kujitakia." THibitisha.

(alama 14)

7. Anwani 'Mstahiki Meya' ni kinaya. Jadili.

(alama 20)

**D: FASIH SIMULIZI**

8. (a) Fafanua sifa tatu za :-

(alm9)

(i) Tendi

(ii) Soga

(iii) Lakabu

(b) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi wa hadithi.

(alm5)

(c) Taja na kueleza vipera vyovoyote vitatu vya hadithi.

(alm6)

ta

ot

151